**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**
# SHULE YA SEKONDARI MKUU
SIMU: 0754601392, 0743361063, 0756776067

S.L.P 145,
**MKUU – ROMBO,**

**Kumb. Na: ……………………………..** **Tarehe: 15/12/2020**

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………
S.L.P……………………………………………….
………………………………………………..……..

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA JANUARI 2021

### 1.0: UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na masomo ya **kidato cha kwanza** katika **shule ya sekondari Mkuu** kwa mwaka **2021**.
Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **29/01/2021**. Aidha siku ya kuja kuripoti njoo na **mzazi/mlezi** wako kwani kutakuwa na fomu maalum ambazo mzazi atatakiwa kujaza, pia kutakuwa na kikao cha wazazi /walezi wote wa wanafunzi kidato cha kwanza tarehe **13/02/2021** unaombwa kufika bila kukosa .

### 2.0 : MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 2.1 : Sare za shule

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni.

**(i) WAVULANA:**

- Suruali mbili (2) rangi **"dark – blue"** za kufungia kiunoni zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili. Angalia kitambaa kilichoambatanishwa.
- Mashati meupe mawili (2) mikono mifupi.
- Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili (2) vya kawaida na viwe vya kamba.
- Soksi aina yoyote nzuri kulingana na viatu vyake.
- T-shirt za shule zinapatikana katika Duka la Shule kwa gharama ya **Tshs: 10,000/=** kwa wale watakaohitaji.
- Mzazi/mlezi mnunulie mwanao sweta rangi ya **dark blue** yenye shingo ya "**V**", aje nayo siku ya kuripoti shuleni.

**(ii) WASICHANA:**

- Ashone sketi mbili (2) rangi ya "**dark – blue"** kwa urefu unaofika kwenye viatu. Angalia kitambaa kilichoambatanishwa. *Mshono – **"Rinder box".**
- Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi
- Anunue viatu jozi mbili rangi nyeusi vya kufunga kwa kamba vya kawaida
- Soksi nyeupe ndefu jozi 2 au zaidi.
- Mzazi/mlezi mnunulie mwanao sweta rangi ya **dark blue** yenye shingo ya "**V**", aje nayo siku ya kuripoti shuleni

  **NB:** Kwa wasichana Waislamu wanaruhusiwa kuvaa shati ya mikono mirefu na **HIJABU** nyeupe. Anunuliwe Hijabu hiyo.
- T-shirt za shule zinapatikana katika Duka la Shule kwa gharama ya **Tshs: 10,000/=** kwa wale watakaohitaji.

### 2.2. MAHITAJI YA MWANAFUNZI DARASANI

- Madaftari makubwa yasiyopungua (11)
- Kalamu, pencil, rula, mkebe wa hesabu pamoja na begi la kubebea vitu hivyo.
- Madaftari madogo kumi na moja (11) kwaajili ya mazoezi.
- Karatasi kwa ajili ya mitihani (rim paper plain A4 nyeupe) moja kwa mwaka.
- Mnunulie mwanao vitabu vya kidato cha kwanza hapa ninapendekeza vilivyochapishwa na oxford na T.I.E. Aidha vitabu vingine ambavyo vinaendana na muhutasari vitafaa.
- Mnunulie mwanao kamusi (dictionary) ya kiingereza.

### 2.3: CHAKULA

Kwa maelekezo ya serikali kila mzazi atamhudumia mtoto wake katika masuala ya chakula. Hivyo wazazi mnatakiwa kulipia kiasi cha Tshs. **81,400/=** kwa mwaka. Pia unaweza kulipa Tshs. **40,700**/= kwa mhula kupitia benki ya **NMB** akaunti namba **40410007859** jina la akaunti ni **AKAUNTI YA CHAKULA MKUU SEKONDARI.**

### 3.0 : MICHANGO MINGINE

Vikao vya wazazi vilivyokaa tarehe 15/7/2017 na tarehe 25/01/2020 viliazimia kuchangia gharama kwa mwaka kama ifuatavyo:-

1. Mchango wa walimu wa Sayansi kwa mwaka ni – **14,000/=** Akaunti Na. **40410007859**.
2. Mchango wa ujenzi wa bweni kwa mwaka ni– **10,000/=** Akaunti Na. **40410007859**.
   **Jina la Akaunti NMB:** ***AKAUNTI YA CHAKULA MKUU SEKONDARI.***
3. Mchango wa mitihani ya kila wiki kwa mwaka ni **– 10,000/=** Akaunti Na. **40410019335**
   Jina la akaunti: **AKAUNTI YA MITIHANI MKUU SEKONDARI**

### 4.0: FOMU MBALIMBALI KWA MZAZI/MLEZI/MWANAFUNZI ZA KUJAZA

Fomu mbalimbali za kujazwa na mwanafunzi/mzazi/mlezi zimeambatanishwa.

**NB:** ***Hakikisha unamfanyia vipimo mwanafunzi katika hospitali ya serikali kwa kutumia fomu iliyoambatanishwa na uwasilishe risiti ya upimaji kutoka katika kituo au hospitali ya serikali siku anayoripoti shuleni.***

### 5.0 : SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE ZIMEAMBATANISHWA

Mwisho tunampongeza tena mwanao kwa kuchaguliwa kwake na tunamkaribisha **Shule ya Sekondari Mkuu.**

**ASANTE NA KARIBU SANA.**

________________

**K. MASHIMBA**
**MKUU WA SHULE**

**NB**: *Mzazi/mlezi unatakiwa kufika shuleni kila mara kufuatilia maendeleo ya mwanao kitaaluma na nidhamu, kutakua na daftari maalumu la kutunza kumbukumbu kwa wazazi wanaofika.*

**( KIAMBATANISHO Na. 1 )**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

**SHERIA ZA SEKONDARI ...................................... (TANZANIA)**

**1. HESHIMA NA UTII**

(i) Ni lazima kila mwanafunzi atii viongozi wote kuanzia walimu, wafanyakazi, viranja na wale wote waliomzidi umri.

(ii) Ni lazima kila mwanafunzi asimame na kusalimu viongozi na wakuu wote na wote waliomzidi umri.

(iii) Ni lazima kila mwanafunzi aitike mara moja na kukimbilia mahali anapoitwa wakati asikiapo kengele au wito mwingine wowote.

(iv) Ni lazima kila mwanafunzi atii maagizo kwanza kabla ya kujenga hoja.

**2. MAHUDHURIO NA KUWAHI**

(i) Ni lazima kila mwanafunzi awepo shuleni muda wote anaotakiwa.

(ii) Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie na kushiriki katika vipindi vyote ndani na nje ya darasa.

(iii) Iwapo mwanafunzi ameshauriwa kutofanya kazi Fulani kwa sababu za kiafya, UTHIBITISHO wa Daktari wa Hospitali ya Serikali utahikajika.

(iv) Mwanafunzi akikosa shule kwa zaidi ya siku tatu (3) mfululizo muhula mmoja bila sababu zenye kukubalika na shule atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja ma kusimamishwa masomo.

**3. UVAAJI WA SARE ZA SHULE**

(i) Ni lazima kila mwanafunzi awe msafi wa mwili na mavazi.

(ii) Sare ya shule ni lazima ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo shuleni na wakati wowote atakapohitajika kuvaa akiwa nje ya shule.

(iii) Mashati na blauzi ni lazima yachomekewe, vishikizo vyote viwepo na kufungwa. (iv) Nywele ziwe fupi na zilizochanwa na nadhifu

**4. MWANAFUNZI HARUHUSIWI:**

(a) Kuwa na ndevu

(b) Kuwa na kucha ndefu

(c) Kupaka nywele au macho au mdomo rangi

(d) Kukaanga nywele (kuweka nywele dawa)

(e) Kuvaa kilemba, kofia, hereni, mkufu, vipuli, pete na mapambomengine mbalimbali.

**5. LUGHA YA MAWASILIANO**

(i) Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza tu isipokuwa kwenye somo la Kiswahili na dini ikibidi. Wanafunzi watawasiliana na watu wengine kwa lugha ya Kiswahili ikibidi.

(ii) NI MARUFUKU kwa mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote.

(iii) Lugha chafu ya matusi HAIRUHUSIWI shuleni.

**6. USAFI WA MAZINGIRA**

(i) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuweka eneo la shule na majengo ya shule katika hali safi.

(ii) Vyoo na ukumbi wa chakula ni lazima viwe safi na vitumiwe ipasavyo.

(iii) Uchafu/takataka ni lazima zitupwe jalalani.

**7. KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE**

(i) NI MARUFUKU kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo au kazi nyingine nje ya darasa bila ruhusa.

Ruhusa itatolewa na mwalimu wa zamu na kuidhinishwa na Mkuu wa shule au makamu mkuu wa shule na kupewa kibali maalumu (*permission slip*) na mara arudipo akirudishe kibali kwa mwalimu wa zamu.

(ii) Mwanafunzi awapo shuleni NI MARUFUKU kutembea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu:

- (a) Chumba cha walimu (Staff-Room)
- (b) Nyumba za walimu na watumishi wasio walimu.
- (c) Ofisi na Stoo za shule.
- (d) Jikoni.
- (e) Karakana na maabara.
- (f) Sehemu zenye mashamba na mifugo.

**8. MICHEZO**

(i) Ni lazima kila mwanafunzi ashiriki katika michezo inayofanyika shuleni. Hivyo awe na nguo za michezo kama viatu(raba), T-Shirt na Bukta au "Truck Suit"

**9. ADHABU ZINAZOTOLEWA NA SHULE**

(i) Kuoywa kwa mdomo wa maandishi.
(ii) Kurudishwa nyumbani kwa muda ama kufukuzwa shule.
(iii) Kuruka kichura.
(iv) Kufanya kazi za nje.
(v) Kufikishwa katika kamati ya nidhamu kwa hatua kali za kinidhamu.
(vi) Kuchapwa viboko (*Kwa idhini ya Mkuu Wa Shule*).

**MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE**

1) Wizi
2) Ulevi wa pombe au madawa ya kulevya
3) Uvutaji bangi/sigara
4) Kuanzisha au kushiriki katika mgomo au fujo za aina yoyote shuleni
5) Kutoheshimu alama za Taifa kama vile Bendera ya Taifa, picha ya Rais ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Makamu wake, Fedha ya Tanzania n.k
6) Uasherati
7) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
8) Kupata mimba au kutoa mimba au kumpa mimba msichana
9) Kuoa au kuolewa
10) Kukataa adhabu iliyotolewa na uongozi wa shule
11) Kupigana au kumshambulia mtu yeyote au kuzomea au lugha ya matusi 12) Kutohudhuria masomo
13) Utoro wa vipindi wa muda mrefu
14) Kukataa kufanya mazoezi ya mitihani
15) Kukataa kufanya usafi wa maeneo shuleni
16) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au kutumia simu shuleni.
17) Mwanafunzi kuwa na radio shuleni. Vyombo vya habari vipo shuleni eg. TV

**( KIAMBATANISHO Na. 2 )**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**


Shule ya Sekondari Mkuu,
TEL: +255 764 613031 S.L.P 145,
TEL: +255 756 776067 **MKUU-ROMBO.**


## KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

### 1. WAJIBU WA MWANAFUNZI ANAYESOMA SEKONDARI

Mwanafunzi yeyote anatakiwa afahamu, azingatie na afuate taratibu zifuatazo:

(i) Kuwa na heshima kwa walimu, Watumishi wengine na wote waliomzidi umri na wadogo.
(ii) Kuongea lugha safi isiyo na matusi wala kashfa kwa binadamu yeyote awaye.
(iii) Kushiriki na kusaidiana katika kazi za shule.
(iv) Kuwahi shule, kufanya kazi zote za shule kuendana na maagizo yatolewayo na uongozi wa shule.
(v) Kuhakikisha kwamba mazingira ya shule anakoishi yanakuwa safi wakati wote, kwa kufanyia usafi.
(vi) Kusimama na kusalimia wakubwa wanapopita mbele yake na walimu wanapoingia darasani.
(vii) Kupokea kwa heshima mizigo kwa watumishi wa shule na wageni wa shule na kuwasaidia.
(viii) Kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, wimbo wa Shule, Nembo za Taifa, Fedha za Taifa, Picha za viongozi wa serikali, n.k.
(ix) Kutii na kuheshimu wito wowote unaotolewa shuleni na kengele inapopigwa.
(x) Kutii na kuheshimu wito na kengele mara tu inapogongwa.
(xi) Kuheshimu mahali pa mikusanyiko kwa utulivu, na kufuata utaratibu uliowekwa.
(xii) Kuheshimu na kutunza Mali za Umma na binafsi.
(xiii) Kusoma kwa bidii, na kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa na Taifa.
(xiv) Kulipa ada na michango mingine ya shule bila kuchelewa.
(xv) Kufuata sheria zote za shule.

### 2. MAMBO AMBAYO HAYARUHUSIWI MWANAFUNZI KUYATENDA

(i) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
(ii) Kufuga kucha, ndevu na Kuvaa herein/bangili, mikufu au viwalo tofauti na sare ya shule awapo shuleni.
(iii) Kunyoa kipara, panki, kupaka rangi midomo/kucha na kujipulizia marashi.
(iv) Kutumia lugha ya matusi au kashfa.
(v) Kutoka nje ya maeneo ya shule bila ruhusa kutoka kwa mwalimu mhusika.
(vi) Kutembea maeneo kama nyumba za watumishi, ofisi za walimu, maabara, maktaba na chumba cha kompyuta bila ruhusa

***Mwanafunzi akienda kinyume na yaliokwisha tajwa hapo juu hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.*



www.mkuutaaluma.blogspot.com

( KIAMBATANISHO Na. 3 )

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Shule ya Sekondari Mkuu,
FAX: +255 27 2757271 S.L.P 145,
TEL: +255 272757271 **MKUU-ROMBO.**

**YAH: MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII**

**1. MWANAFUNZI**

Mimi …………………………………………………..……………..………..…………………………… (jina la mwanafunzi),

Ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa yote kwenye maelekezo ya kujiunga na shule hii, na **nitayazingatia** kwa muda wangu wote wa masomo yangu hapa shuleni. **Nitakubali kurekebishwa na walezi** endapo nitakwenda kinyume na melekezo hayo kwani maelekezo hayo ndiyo yatakayonifanya **nisome kwa bidii** na kufaulu mitihani yote itakayotolewa na Shule/Wilaya/Mkoa/Kanda/Taifa shuleni.

……………………………………… ………..………………………

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** **TAREHE**

**2. MZAZI/MLEZI**

Mimi ........................................................................................................ (Jina kamili la mzazi/mlezi), ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………………………………………..…………………..……… (jina la mtoto anayejiunga na shule).

Ninakiri kupokea, Kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizoko kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Mkuu. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo **nitakua tayari kukubali** hatua zitakazochukuliwa dhidi yake, ili kumwepushia usumbufu. Nitakamilisha kila mwanzo wa muhula **mahitaji yake yote ya shule** ikiwa ni pamoja na **ada na michango** mbalimbali ya shule.

…………………………………

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI WA KIUME**

**Tarehe: …………………………**

**Simu: ……………………………………..….**

…………………………….

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI WA KIKE**

**Tarehe: …………………………**

**Simu: ………………..……………….**



*www.mkuutaaluma.blogspot.com*

**(KIAMBATANISHO Na. 4)**

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MKUU SECONDARY SCHOOL

# MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical Officer in a Government hospital in respect of all new students to Mkuu Secondary School.

STUDENT'S FULL NAME: ……………………………………………………………………….

AGE: ………………………………………………………..

1. Blood count (Red and White): ………………………………………………
2. Stool Examination: ………………………………………………………………………
3. Urine Examination: …………………………………………………………………….
4. Eye test: ………………………………………………………………
5. Ear test: …………………………………………
6. Speech test: ……………………………………………………………………
7. T.B test: ………………………………………………………………………………………
8. STD test: ………………………………………………………………………………………
9. Spleen: ……………………………………………………………………………………………
10. Abdomen: ……………………………………………………………………………………..
11. Additional information from any Physical, Mental, Hereditary diseases or disabilities:

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

*Treatment after Examination*:

……………………………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**

*I certify that the above-mentioned student has been thoroughly examined by me and found fit/unfit to pursue further education.*

*SIGNATURE*: ……………………………………………………………………………….

*DESIGNATION/STAMP*……………………………………………………………………….

*DATE*: ………………………………………………………………..

*STATION*: ……………………………………………………………